JIUNGE NA MASOMO YA SAYANSI

Chagua Ukunga

“Naupenda ukunga, ni Chaguo langu!”

“Wakina mama hawafi kwasababu ya magonjwa tunayoshindwa kuyatibu; wanakufa kwasababu jamii hazijaamua kuona umuhimu wa kuokoa maisha yao” (Muhamed Fatah 2004

KAMPENI YA KUUTANGAZA UKUNGA KAMA TASNIA INAYOOKOA MAISHA

Malengo ya kampeni hii ni:

- Kuwahimiza wanafunzi wa shule za sekondari kusoma masomo ya sayansi ili kuwawezesha kuwa wakunga
- Kuwafikia wanafunzi wengi wa shule za sekondari hasa hasa mkoa wa Mtwara
- Kuwashirikisha wadau na washirika wengine katika kuifikisha kampeni hii katika mikoa mingine ya Nyanda za Juu Kusini
- Kuifikia na kuhamasisha Wizara ya Afya na Maendeleo ya Jamii na watendaji wa ngazi za mikoa na wilaya kuweza kupanga na kutenga bajeti za kuwasomesha wakunga katika vitengo vyao

Kila mama anahitaji uzazi salama

Kila mwaka wanawake nusu milioni duniani kote hufariki wakiwa wajawazito na wakati wakijifungua, watoto milioni 4 huzaliwa wakiwa wamekufa, na milioni nne wengine hufariki kabla ya kutimiza mwezi mmoja. Chakusikitisha zaidi, asilimia 99 ya vifo hivi hutokea katika nchi zilizo na vipato vya chini na vya kati. Idadi kubwa ya wanawake hawa huzalia nyumbani, mara nyingi wakiwa wenyewe na hata bila msaada wa kitaalam.

Kwa Tanzania hali ya uzazi wa akina mama na vifo vya watoto ni kama ifuatavyo:

- Uwiano wa vifo vya akina mama na watoto ni 454 kwa kila 100,000 wanozaliwa; Hii inamaanisha takribani wakina mama 8000 hufa kila mwaka wakati wa ujauzito na wa kujifungua kutokana na sababu zinazoweza kuzuilika.
- Uwiano wa Vifo vya watoto walio chini ya miaka mitano ni 81 kwa kila vizazi hai 1000; watoto wanaokufa wakati wa kujifungua ni 26 kwa kila vizazi hai 1000 na vifo vya watoto wachanga ni 51 kwa kila vizazi hai 1000.
- Ni asilimia 51 tu ya kina mama wajawazito wanaojifungulia katika vituo vya afya.
- Upatikanaji wa huduma za kitaalum za uzazi ni asilimia 49 tu (DHS 2010).
- Mkunga mmoja (1) anatoa huduma kwa akina mama 500 ukilinganisha na uwiano wa viwango vya Shirika la Afya duniani ambao ni mkunga 1 kwa wakina mama 6 (WHO 2005)

HALI HAITAKIWI KUWA HIVI:

Tukiwa na wakunga wenye ujuzi, wenye vifaa na msaada wanaohitaji, wanaweza kuleta mabadiliko kati ya maisha na kifo kwa wanawake takribani 300,000 kila mwkaa na mara kumi kwa vichanga vyao. (UNFPA, 2013)

WAKUNGA WANAFANYA NINI?

Huduma za msingi zitolewazo na wakunga ni pamoja na:

1. Kutoa huduma rafiki za afya ya uzazi kwa vijana.
2. Kutoa huduma,ushauri na elimu ya afya kabla ya kujifungua.
3. Kuwapa huduma wakina mama wakati wa ujauzito, kujifungua na baada ya kujifungua.
4. Kutibu matatizo yoyote yanayojitokeza kuhusiana na kubomoka kwa ujauzito na/au utoaji mimba.
5. Kutoa huduma kwa kichanga.
6. Kutambua na kushughulikia matatizo ya akina mama na vichanga kabla, wakati na baada ya kujifungua.
7. Kutoa huduma zote za afya na taarifa, ikiwa ni pamoja na afya ya uzazi na uzazi wa mpango.
8. Kuwasasidia akina mama kunyonyesha kwa usalama na kiafya.
9. Kuwasimamia au kuwawahisha kwa wataalamu zaidi akina mama na watoto wachanga kwa huduma zaidi za kiafya pale tatizo linapotokea wakati wa ujauzito au wakati wa kujifungua.
10. Kutoa huduma nyinginezo za kiafya kwa jamii kama chanjo na matibabu ya magonjwa ya kawaida yanayohusiana na afya ya uzazi.

KUSOMA MASOMO YA SAYANSI

" Soma sayansi uwe mkunga mtaaluma!"
"Soma sayansi uutambue mwili wako!"
"Jiunge na masomo ya sayansi uokoe maisha!"
"Maisha ni Sayansi: Jiunge na Sayansi!"
"Jiunge na Sayansi Ufanikiwe Maishani!"

UKUNGA KAMA TASNIA

MKUNGA NI NANI?

Mkunga ni mtu yeyote ambaye amehitimu elimu ya ukunga ambayo inatambulika katika nchi husika na ambayo ipo katika taratibu za kiutendaji za Baraza la Kimataifa la Wakunga (ICM) pamoja na mfumo wa kiutendaji na viwango vya elimu ya ukunga; ambaye amepata kibali cha kukidhi na kusajiliwa au kuruhusiwa kisheria kutoa huduma za ukunga na kuitwa "Mkunga" na anayeonesha weledi katika kazi ya ukunga

"Mimi Mkunga ndiye wa kwanza duniani kukubeba mikononi!"

"Mimi ni mkunga: Karibu duniani!"
"Naupenda ukunga, ni Chaguo langu!"
"Ukunga, taaluma yenye uwanda mpana kiajira duniani kote!"

"Jiunge na tasnia ya ukunga; Okoa maisha!"

HUDUMA ZA AFYA YA UZAZI NA HAKI KWA VIJANA

Huduma za afya ya uzazi na haki ni nini?

Haki za afya ya uzazi ni pale ambapo vijana wana taarifa sahihi na hivyo wana mitazamo na tabia sahihi juu ya mchakato mzima wa afya ya uzazi. Wana uwezo wa kutambua uwezo wao binafsi katika mazingira tata ya kimaendeleo kuhusiana na jinsi. Mazingira haya ni pamoja na; kuukubali mwili wake, kutambua utofauti wa kijinsi; kuwa na uelewa stahikijuu ya uumbwaji na maumbile ya binadamu; kuwasiliana kwa ufasaha na familia; kuelewa marafiki; kutambua vitu au mazingira hatarishi, majukumu, na matokeo ya matendo ya kingono; ana uelewa stahiki juu ya namna ya kuchukua hatua za kujikinga na mazingira hatarishi; ana ufahamu juu ya wapi na namna ya kupata na kuzitumia taarifa na huduma za kiafya, mifumo na taasisi za kijamii za kiafya kadiri zinavyohitajika; kujiwekea mipaka sahihi ya kingono; kutenda kwa kujitambua kwa kufuata misingi ya kibinadamu na thamani yake; na kuunda na kuiendeleza mahusiano yenye kufuata afya na yenye tija. Wanawake na wanaume wote wanapaswa kuvijua vigezo mbalimbali vya afya ya uzazi vikiwemo vifuatavyo:

"Huduma za Afya ya Uzazi ni Haki yako; Zitafute!"
"Bikra yangu, Faraja yangu!"
"Mtembelee mkunga kwa huduma rafiki za afya ya uzazi kwa vijana!"
"Jiunge na ukunga uongeze huduma rafiki za afya ya uzazi kwa vijana!"
"Naipenda jinsi yangu!"
"Ni Sawa kusema HAPANA kufanya ngono!
"Nina haki ya kupata elimu: Nijulishe juu ya afya ya uzazi!"
"Maambukizi ya VVU kwa vijana ni asilimia 60: Chukua Hatua!"
"Unaweza kuchagua kupunguza maambukizi ya VVU!"
"Amka, Shiriki, Badili mtazamo na jifunze juu ya Afya ya Uzazi!"
"Nina haki ya kuamua ni lini nioe/niolewe!"
"Nina haki ya kujua kuhusu mwili wangu!"
"Nina haki ya kuamua maisha yangu ya baadae!"
"Ulevi na madawa ya kulevya ni hatari kwa Afya bora ya uzazi; Epuka!"

NINI KIFANYWE NA WATUNGA SERA KATIKA NGAZI ZA SERIKALI KUU NA SERIKALI ZA MITAA?

Ujumbe juu ya kuongeza bajeti na kuwasomesha wakunga na pia kuupa kipaumbele ukunga kama taaluma. Mfano umetolewa kwa mradi wa "Stand up for African Mothers" huko Kilindi ambapo hadi sasa wanafunzi 10 wamewezeshwa na wadau na wafadhili mbalimbali ili kupata elimu ya ukunga katika Shule ya Uuguzi na Ukunga Korogwe, kwa makubaliano kuwa wakihitimu watarudi kufanya kazi katika wilaya ya Kilindi (AMREF 2013). Mradi unalenga kuwafundisha wakunga ili kuokoa maisha.

PMO-RALG na Wizara ya Afya na Maendeleo ya Jamii: Kuwafanya wakunga na kuufanya ukunga kipaumbele katika nyanja za utengenezaji bajeti na kutenga fedha za kutoa mafunzo na pia kuajiri wakunga:

Baraza la halmashauri na Mkurugenzi: Watambue na kuipa kipaumbele taaluma ya ukunga katika mipango ya maendeleo ya halmashauri)

Baraza la halmashauri na Mkurugenzi: Kuongeza bajeti kwa ajili ya kutoa mafunzo na kuwapa uwezo wakunga katika vituo vyao (katika halmashauri husika) ili kuwajengea mazingira rafiki ya kuendelea kuwepo.

Baraza la halmashauri na Mkurugenzi: Kuboresha ufundishwaji wa masomo ya sayansi katika shule za sekondari katika halmashauri husika

Baraza la halmashauri: Kuhakikisha ni wataaluma wa huduma za afya pekee hasa katika ukunga ndio watakaoajiriwa ili kuokoa maisha na kutoa huduma za kiafya

Watendaji wa kata na vijiji:

1. Watambue huduma bora za uzazi kwa akina mama ni jukumu la kila mmoja; Dai watoa huduma za afya ambao ni wataaluma hasa hasa wakunga.
2. Jamii: Hakikisha wakina mama wajawazito wanapata huduma za wakunga wataalum
3. Mama mwenye afya hulea mtoto mwenye afya na taifa linakuwa na afya

The White Ribbon Alliance For Safe Motherhood Tanzania

WRATZ mawasiliano: Kwa maelezo zaidi ya WRATZ na kupata fomu ya uanachama, tafadhali wasiliana na:

Muungano wa Utepe Mweupe wa Uzazi Salama Tanzania (WRATZ)
Barua pepe: rose.mlay@gmail.com, Simu ya mkononi: 255 754 316 369
Tovuti: www.whiteribbonalliance.org

Kwa maelezo zaidi ya TAMA tafadhali wasiliana na: General Secretary,
Tanzania Midwives Association, P.O.Box 65004,
Barua pepe: seolesh@yahoo.com, Simu ya mkononi: +255 784 287062

Asasi Wanachama wa WRATZ